# TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA

JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI

MTAALA WA SHULE ZA MSINGI

Gredi 2

Chapisho la Kwanza 2017

Chapisho la Pili 2022

Chapisho la Tatu 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

ISBN:
Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

## YALIYOMO

MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ........ iv
LESSON ALLOCATION AT LOWER PRIMARY ........ vii
MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA MASOMO YA MSINGI ........ viii
KAULI KIINI ........ ix
MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI ........ ix
1.0 SHULENI ........ 1
2.0 HAKI ZANGU ........ 9
3.0 LISHE BORA ........ 19
4.0 USAFIRI ........ 29
5.0 MNYAMA NIMPENDAYE ........ 37
6.0 UKOO ........ 45
7.0 SEBULENI ........ 53
8.0 USALAMA WANGU ........ 61
9.0 HOSPITALINI ........ 69
10.0 HALI YA ANGA ........ 78
MWONGOZO WA KUTATHMINIA STADI ZA LUGHA GREDI YA 2 ........ 86
APPENDIX I: SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL) ........ 93

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.
   a) **Mahitaji ya kijamii**
      Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
      Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
      Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda.
      Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa. Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira.**
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa

kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

**LESSON ALLOCATION AT LOWER PRIMARY**

| S/No | Learning Area | Number of Lessons |
|---|---|---|
| 1. | Indigenous Language Activities | 2 |
| 2. | Kiswahili Language Activities / Kenya Sign Language Activities | 4 |
| 3. | English Language Activities | 5 |
| 4. | Mathematical Activities | 5 |
| 5. | Religious Education Activities | 3 |
| 6. | Environmental Activities | 4 |
| 7. | Creative Activities | 7 |
| 8. | Pastoral/Religious Instruction Programme | 1 |
| **Total** | | **31** |

**MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA MASOMO YA MSINGI**

Kufikia mwisho wa masomo ya msingi gredi, mwanafunzi aweze:

a) kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake
b) kudhihirisha ufasaha wa dhana malimbali kusuluhisha matatizo ya kila siku,
c) kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya Kiswahili
d) kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji
e) kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano
f) kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana
g) kuonyesha ukakamavu katika kuwasilisha masuala yanayomkabili na yanayokabili mazingira yake.

**KAULI KIINI**

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya na lugha ya mawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wakenya wengi hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu wanafunzi wapate umilisi wa kuwasiliana kwa Kiswahili mapema hasa katika shule za msingi. Somo hili humwezesha mwanafunzi kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Aidha, somo hili humwandaa mwanafunzi kwa mafunzo ya viwango vya juu na baadaye katika ajira.

**MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI**

Kufikia mwisho wa kiwango cha chini, mwanafunzi aweze:

a) Kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano.
b) Kuzingatia kanuni za lugha ili kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi.
c) Kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali.
d) Kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani.
e) Kutumia hati za kimaandishi na mfumo wa kidijitali kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali.
f) Kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

MADA
Kusikiliza na Kuzungumza
Kusoma
Kuandika
Sarufi

Mada Ndogo

| Mada | **Mada Ndogo** |
|---|---|
| Kusikiliza na Kuzungumza | Maamkuzi na Maagano |
| | Matamshi Bora |
| | Maneno ya Heshima na Adabu |
| | Matamshi Bora |
| | Hadithi |
| | Matamshi Bora |
| | Maagizo |
| | Matamshi Bora |
| | Mazungumzo ya papo kwa hapo |
| | Matamshi Bora |
| Kusoma | Kusoma Ufahamu |
| | Kusoma kwa Ufasaha |
| | Kusoma kwa Ufahamu |
| | Kusoma kwa Ufasaha |
| | Kusoma kwa Ufahamu |
| | Kusoma kwa Ufasaha |
| | Kusoma kwa Ufahamu |
| | Kusoma kwa Ufasaha |

| | |
|---|---|
| | Kusoma kwa Ufahamu |
| | Kusoma kwa Ufasaha |
| Kuandika | Hati nadhifu: Sentensi |
| | Hati Nadhifu Herufi kubwa |
| | Mpangilio wa Herufi Ndogo |
| | Nafasi katika maandishi. |
| | Uakifishi: Matumizi ya Kiulizi |
| | Tahajia Imla |
| | Uhariri |
| | Tahajia |
| | Kuandika Kifungu |
| | Maneno na Sentensi |
| Sarufi | Matumizi ya wewe na nyinyi |
| | Umoja na Wingi wa Vifungu |
| | Matumizi ya Huyo na Hao |
| | Umoja na wingi wa vifungu vya maneno |
| | Matumizi ya -ako na -enu |
| | Matumizi ya: (-refu, - kubwa, - tamu) |
| | Ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi |
| | Matumizi ya huu na hii |
| | Matumizi ya vizuri na vibaya, polepole na haraka |
| | Vinyume vya Vitendo |

Matokeo ya Kijumla Yanayotarajiwa Katika Kiwango cha Kwanza cha Masomo Kufikia mwisho wa kiwango cha kwanza cha masomo, mwanafunzi aweze:

a) kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake
b) kudhihirisha ufasaha wa kuzungumza kwa Kiswahili
c) kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya Kiswahili
d) kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji
e) kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano
f) kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana
g) kuonyesha ukakamavu katika kuwasilisha masuala yanayomkabili na yanayokabili mazingira yake.

| **1.0 SHULENI** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Maamkuzi na Maagano** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maamkuzi na maagano ya nyakati za siku,<br>b) kuamkua na kuitikia maamkuzi na maagano ya nyakati za siku,<br>c) kufurahia kuamkua na kuagana ili kujenga mshikamano wa kijamii. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi mbalimbali ya nyakati za siku (*habari ya asubuhi, habari ya mchana, Habari ya jioni, siku njema*) kutoka kwenye chati, vitabu, kadi maneno, mti maneno, michoro, picha au vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kutazama picha za watu wakisalimiana na kuagana akishirikiana na wenzake kujadili picha hizo,<br>● kutazama video inayoonyesha watu wakitumia maamkuzi na maagano ya nyakati za siku,<br>● kuigiza na mwenzake maamkuzi na maagano mbalimbali. | Tunaamkuana vipi wakati wa asubuhi, mchana na jioni? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika kazi ya kikundi na kujadiliana kuhusu maamkuzi na maagano ya nyakati za siku.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama watu wakisalimiana na kuagana.<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapoigiza ipasavyo maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali. | | | | |

| |
|---|
| ● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapojadili picha za watu wanaoamkuana na kuagana. |
| **Maadili:**<br>● Heshima – mwanafunzi anapowaamkua wengine kwa heshima.<br>● Upendo – mwanafunzi anapowaamkua na kuwaaga wenzake.<br>● Amani - mwanafunzi anapowamkua na kuwaaga wenzake. |
| **Suala mtambuko:** Mshikamano wa kijamii-mwanafunzi anapoigiza na wenzake maamkuzi na maagano darasani, shuleni na katika mazingira yake. |

| 1.0 SHULENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **1.2** | **1.2.1 Kusoma Ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 31 - 34 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v shule, mwalimu, mwanafunzi, gwaride, afisi, darasa, , uwanja, gredi, dawati, kifutio, n.k)* akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake | Kusoma kifungu ili ufahamuujumbe unafanya nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuchangia katika kutambua msamiati, kutabiri na kujibu maswali.
- Uwazaji wa kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotoa utabiri kutokana na picha na kuchangia katika kujibu maswali.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kusoma hadithi na kutazama picha.

**Maadili:**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kikundi kujadiliana.
- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji - mwanafunzi anapoeleza mafunzo kutokana na kifungu kuhusu suala lengwa.

**Masuala mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma hadithi na pia kujadili picha ukakamavu wake unaimarika.
- Utunzaji na matumizi yafaayo ya vitu vinavyopatikana shuleni - mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa

**Uhusiano na masomo mengine:** Language activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma

| 1.0 SHULENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Hati nadhifu: Sentensi** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua hati nadhifu katika sentensi,<br>b) kuandika sentensi akizingatia hati nadhifu,<br>c) kufurahia kuandika akizingatia hati nadhifu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua hati nadhifu kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>• kujadili na wenzake kuhusu hati nadhifu kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali,<br>• kuandika sentensi fupi kuhusu suala lengwa akizingatia: (*maumbo yanayofaa, kutoacha nafasi baina ya herufi katika neno, kuacha nafasi kati ya neno la lingine*),<br>• kuwasilisha darasani sentensi zake ili wenzake wamtolee maoni,<br>• kumwandikia mzazi au mlezi sentensi fupi kuhusu suala lengwa akizingatia hati nadhifu. | Je, ni mambo gani unayozingatia wakati wa kuandika? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu hati nadhifu. Pia, anaposhiriki kikamilifu kuandika akiwa na wenzake katika kikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotambua hati nadhifu katika kifaa cha kidijitali.<br>• Kujiamini – mwanafunzi anapoandika akizingatia hati nadhifu. |
| **Maadili:**<br>• Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli ya kuandika.<br>• Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Mahusiano ya kijamii – mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu hati nadhifu uwezo wake wa uandishi bora unakuzwa.<br>• Usalama mtandaoni – mwanafunzi azingatie hatua za kiusalama anapotambua hati nadhifu kwenye kifaa cha kidijitali. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Masomo yote ya mtaala gredi ya 2 - masomo yote ya mtaala yanasisitiza hati nadhifu. |

| 1.0 SHULENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Liyopendekezwa** |
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Matumizi ya wewe na nyinyi** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua **wewe** na **nyinyi** katika sentensi,<br>b) kutumia **wewe** na **nyinyi** ipasavyo katika sentensi,<br>c) kufurahia kutumia **wewe** na **nyinyi** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusikiliza kifungu au wimbo unaohusu nafsi ya pili (**wewe** na **nyinyi**), kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali,<br>• kusoma vifungu vilivyo na nafsi ya pili (**wewe** na **nyinyi**) akishirikiana na wenzake,<br>• kutumia nafsi ya pili (**wewe** na **nyinyi**) umoja na wingi kwa kuigiza mazungumzo na wenzake katika kikundi (*k.m: Wewe unasoma - Nyinyi mnasoma; Wewe ulienda shuleni - Nyinyi mlienda shuleni.),*<br>• kujaza nafasi kwa kutumia wewe na **nyinyi,**<br>• kutaja zoezi la nafsi ya pili kwenye tarakilishi kwa kuburura majibu sahihi na kujaza nafasi akielekezwa na mwalimu,<br>• kuwasiliana na mzazi au mlezi wake kwa kutumia nafsi ya pili **(wewe** na | Ni neno gani unaloweza kutumia kuwataja wenzako bila kutaja majina yao? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **nyinyi**). | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kutoa mifano kwa kutumia **wewe** na **nyinyi.**
- Ubunifu – mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **wewe** na **nyinyi**.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya **wewe** na **nyinyi.**
- Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutumia wewe na **nyinyi** ifaavyo.

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika kuigiza matumizi ya wewe na mimi na kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
- Heshima – mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake na kuwapatia nafasi kushiriki katika majadiliano.
- Upendo – mwanafunzi anapokuwa tayari kushirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.

**Suala Mtambuko:** Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kuigiza mazungumzo ya nafsi ya pili **wewe** na **nyinyi.**

**Uhusiano na masomo mengine:** English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yana mada kuhusu nafsi.

| 2.0 HAKI ZANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Llililopendekezwa** |
| **2.1**<br>**Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1**<br>**Matamshi Bora: Sauti /p/, /f/, /v/**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maandishi,<br>b) kutamka ipasavyo silabi za sauti lengwa katika maandishi,<br>c) kutamka maneno mepesi yanayotokana na sauti lengwa katika maandishi,<br>d) kusoma ipasavyo sentensi nyepesi zenye sauti lengwa kwa matamshi bora | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi kwenye maneno yenye sauti lengwa (/p/, /f/, /v/) katika sentensi akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza silabi lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwaalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka silabi za sauti lengwa akiwa peke yake au na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka maneno yenye sauti lengwa yaliyotamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali akiwa peke yake, au na wenzake akizingatia matamshi bora,<br>● kusikiliza sentensi zenye sauti lengwa zikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali, | Je, kwa nini ni vizuri kutamka maneno vizuri tunapozungumza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuchangamkia usomaji bora wa maneno yanayotumia sauti lengwa katika mawasiliano.. | ● kusoma sentensi za sauti lengwa zilizosomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake kwa kuzingatia matamshi bora,<br>● kujirekodi kwa kutumia kifaa cha kidijitali akitamka sentensi za sauti lengwa na kuwatumia wenzake ili watathmini,<br>● kukariri mashairi na nyimbo katika tamasha za mziki au kwenye hafla shuleni ili kuboresha matamshi kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>● kuwasiliana na mzazi au mlezi wake kwa kutumia maneno yenye sauti lengwa. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapojirekodi akisoma sentensi na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotamka sauti lengwa ipasavyo darasani.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kutamka sauti lengwa katika sentensi.
- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi na kuwakosoa kwa heshima.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko**<br>● Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujirekodi na kutumia wenzake azingatie hatua za kiusalama.<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake darasani kutamka sauti lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>● English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora. |

| 2.0 HAKI ZANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Llililopendekezwa** |
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa ufasaha** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yenye sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yenye sauti lengwa (/p/, /f/, /v/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kuhusu haki za mtoto (*k.v. upendo, mavazi, makao, chakula*) kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 33 kwa dakika) na kwa kuzingatia viakifishi,<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa | Je, ni mambo ganiunavyozingatia ili kusoma kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | cha kidijtali akiwa peke yake, au na wenzake, akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zinazofaa,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutambua sauti na kusoma maneno na sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma maneno na sentensi zenye sauti lengwa.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoendelea kutunga na kusoma sentensi nyepesi zenye maneno ya sauti lengwa.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kutoa mchango wao.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anapotangamana na kushirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapochukua majukumu mbalimbali katika kazi ya kikundi.

**Masuala mtambuko**

- Haki za watoto - mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu haki za watoto akizingatia matamshi bora,kasi ifaayo,sauti inayosikika na ishara zifaazo.
- Afyaa ya mtu binafsi – mwanafunzi anaposoma kifungu kinachuzungumzia suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

Indigenous Language Activities na English Language Activities - masomo haya pia yanashughulikia kusoma

| 2.0 HAKI ZANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Hati Nadhifu: Herufi Kubwa**<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mpangilio ufaao wa herufi kubwa katika matini,<br>b) kuandika herufi kubwa ipasavyo katika maneno na sentensi,<br>c) kufurahia kutumia herufi kubwa ipasavyo katika maneno na sentensi ili kuboresha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mpangilio ufaao wa herufi kubwa katika matini *(k.v. kadi maneno, mti maneno, picha, chati, kitabu, kifaa cha kidijitali, n.k.)* akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kunakili maneno na sentensi kuhusu mada lengwa *(k.v upendo, kupata elimu, chakula, mavazi, makazi)* kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa,<br>● kutunga na kuandika sentensi fupi akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa,<br>● kushirikiana na wenzake kutathmini sentensi walizotunga,<br>● kumwandikia mzazi au mlezi maneno kwa kutumia mpangilio ufaao wa herufi kubwa na hati nadhifu. | Je herufi kubwa huwa sifa gani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapofaulu kuwaonyesha wenzake herufi kubwa ilipotumiwa katika maneno na sentensi. Pia anaposhiriki kutambua na kuandika herufi kubwa katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapoandika herufi kubwa katika maneno na sentensi akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomwandikia mlezi au mzazi wake maneno kwa kutumia herufi kubwa ipasavyo.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Utunzi na usalama wa watoto – mwanafunzi anaponakili maneno na sentensi kuhusu haki za watoto kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa herufi.
- Elimu ya afya ya kujikinga – mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia matumizi ya herufi kubwa katika maneno na sentensi.

| 2.0 HAKI ZANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Liyopendekezwa** |
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Umoja na Wingi wa Vifungu** *(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi,<br>b) kuandika vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia vifungu vya maneno katika umoja na wingi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi (*k.m. haki yangu - haki zetu; mtoto wangu - watoto wetu; nguo yangu - nguo zetu; nyumba yangu - nyumba zetu*) katika matini mbalimbali, kadi maneno, mti maneno, vifaa vya kidijitali n.k,<br>• kuandika vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>• kujaza nafasi kwa kukamilisha vifungu vya maneno katika umoja na wingi akishirikiana na | Umoja na wingi wa vifungu huwa na sifa gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake,<br>● kushiriki katika mchezo wa kupanga kadi za vifungu vya maneno akiambatanisha umoja na wingi,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi wake vifungu vya maneno alivyoviandika kwa umoja na wingi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuandika vifungu vya maneno.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapojenga hamu ya kutaka kueleza kuhusu vitu katika mazingira yake kwa umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kuandika vifungu vya maneno katika umoja na wingi.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuandika vifungu vya maneno katika umoja na wingi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali ipasavyo.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kuandika vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi.<br>● Haki za watoto – mwanafunzi anaposhiriki kuandika sentensi kuhusu haki za watoto. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yana mada zinazohusu umoja na wingi. |

| 3.0 LISHE BORA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Maneno ya Heshima na Adabu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima na adabu yanayotumiwa katika jamii,<br>b) kutumia ipasavyo maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano akiambatanisha na hisia zifaazo,<br>c) Kuthamini | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno ya heshima na adabu *(k.m hodi, karibu, tafadhali, ninaomba, nisamehe na nashukuru)* yanayotumiwa katika jamii,<br>● kujadili ni lini maneno husika yanatumiwa katika mawasiliano akiwa na wenzake,<br>● kutazama michoro mbalimbali na kujadili neno linalofaa kutumiwa katika miktadha husika *(k.m mtoto akibisha mlango, mtu akimkosea mwenzake n.k.),*<br>● kutazama video kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu *(k.m.* | Maneno ya adabu huwa na sifa gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano ya kila siku. | *Mwalimu akimpa mwanafunzi zawadi naye mwanafunzi akishukuru*),<br>● kuambatanisha matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mazungumzo na hisia katika maigizo,<br>● kuwasiliana na mzazi au mlezi kwa kutumia maneno ya adabu na heshima ifaavyo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika majadiliano kuhusu maneno ya heshima na adabu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama maigizo kuhusu vitendo vya heshima na adabu.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoigiza kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.
- Uraia - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili matumizi ya maneno ya heshima na adabu.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapotumia maneno ya heshima na adabu.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kutoa hoja zao katika kikundi na pia anapotumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano.<br>● Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapotazama video kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu azingatie hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities, Indigenous Language Activities na Religious Education Activities – masomo haya pia yanashughulikia dhana ya heshima na adabu. |

| 3.0 LISHE BORA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa ufahamu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 35 - 38 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(afya, nguvu, protini, wanga, vitamini )* akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu cha hadithi kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake, | Je unazingatia nini ilikupata ujumbe katika ufahamu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi<br>• kifungu chepesi cha hadithi kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kuchangia kikamilifu katika kueleza ujumbe wa kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali kutazama picha na kusoma kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake na kumweleza ujumbe katika kifungu chepesi.
- Uwazaji kwa kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotabiri na kufikia uamuzi wa mafunzo anayopata kwenye kifungu cha ufahamu.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi kujadili ujumbe na kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi.
- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachotumia kujifunzia.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya afya ya kujikinga– mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi cha hadithi na kutumia msamiati kuhusu lishe bora,ujuzi wake wa kujikinga dhidi ya maradhi mbalimbali unapanuka.
- Afya ya mtu binafsi – mwanafunzi anasoma matini kuhusu suala lengwa kuhusu lishe bora.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities, Indigenous Language Activities na Environmental Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu.

<table>
<tr><th colspan="5">3.0 LISHE BORA</th></tr>
<tr><th>Mada</th><th>Mada Ndogo</th><th>Matokeo maalum Yanayotarajiwa</th><th>Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa</th><th>Swali Dadisi Lililopendekezwa</th></tr>
<tr><td>3.3 Kuandika</td><td>3.3.1 Mpangilio wa Herufi Ndogo<br>(Vipindi 3)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mpangilio ufaao wa herufi ndogo katika maandishi,<br>b) kuandika kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo,<br>c) kuchangamkia kuandika vifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo ili kufanikisha mawasiliano.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mpangilio ufaao wa herufi ndogo katika maandishi kwenye kadi maneno, chati, daftari au kifaa cha kidijitali,<br>● kuwaonyesha wenzake mpangilio ufaao wa herufi ndogo kwenye kadi maneno, kitabu, chati au kifaa cha kidijitali,<br>● kunakili kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo,<br>● kutunga kifungu kuhusu suala lengwa akizingatia mpangiliounaofaa.</td><td>Kwa nini ni vizuri kuandika herufi ndogo ipasavyo?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kuandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha maneno akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kuandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufu ndogo.</td></tr>
</table>

| **Maadili** |
| --- |
| ● Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuthamini maoni ya wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Mahusiano ya kijamii– mwanafunzi anapowathamini wenzake kutoka jamii mbalimbali wanaposhirikiana kunakili kifungu wakizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo.<br>● |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>● English Language Activities na Indigenous Language Activities – Masomo haya yanafunza uandishi unaozingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo.<br>. |

| 3.0 LISHE BORA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.4 Sarufi** | 3.4.1 Matumizi ya **Huyo** na **Hao** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **huyo** na **hao** katika kifungu,<br>b) kutumia **huyo** na **hao** katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **huyo** na **hao** katika maawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **huyo** na **hao** kwa kutumia nyenzo kama vile kadi maneno, mti maneno, kapu maneno au chati,<br>● kusilikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya **huyo** na **hao** katika kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua **huyo** na **hao** katika kifungu au wimbo aliosikiliza kwa kuongozwa na mwalimu,<br>● kusoma sentensi zenye kudhihirisha matumizi ya **huyo** na **hao** kama vile: ***Huyo** anakula chakula.*<br>***Hao** wanakula chakula.*<br>● kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia huyo na hao,<br>● kumtungia mwenzake katika | Ni maneno gani yatatumiwakuonenyesha mwenzako akiwa mbali kidogo?<br>gani kuonyeshea mwenzako akiwa mbali kidogo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kikundi sentensi kwa kutumia **huyu** na **hao,**<br>● kuandika sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **huyo** na **hao** kama vile: *Huyo ni nani? – Huyo ni kaka.,*<br>● kujaza nafasi kwa kutumia **huyo** na **hao** akielekezwa na mwalimu. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia **huyo** na **hao**.
- Kujiamini – mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **huyo** na **hao** akishirikiana na wenzake katika kikundi.
- Ubunifu - mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia huyo na **hao** kwa lugha fasaha.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kurejelea watu wa familia yake kwa kutumia **huyo** na **hao** ipasavyo.

.**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **huyo** na **hao.**
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapojitolea kumshirikisha mzazi au mlezi wake katika kurejelea watu wa familia yake kwa kutumia maneno **huyu** na **hao**.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>● Utangamano wa kijamii - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu wenye upungufu wa lishe bora kwa kutumia **huyo** na **hao.**<br>● |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>● English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia hushughulikia mada kuhusu vivumishi vya nafsi. |

| 4.0 USAFIRI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Liliyopendekezwa** |
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Matamshi Bora**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa akizingatia matamshi bora,<br>d) kufurahia matamshi bo katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa *(/ch/* na */dh/*) katika maneno kwenye kadi maneno, chati, mti maneno, sentensi, au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kukishirikiana na utumia kifaa cha kidijitali *(k.v. kupitia programu ya papaya)* kusikiliza matamshi bora ya silabi za sauti lengwa,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakisomwa na wenzake darasani kisha kutambua sauti hizo katika maneno hayo,<br>● kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa ifaavyo akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya silabi za sauti lengwa kutoka kwa kitabu au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake. | Je, ni maneno gani unayojua yenye sauti /ch/ na /dh/? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali akisoma kifungu na kutamka sauti lengwa ipasavyo.<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kutamka sauti lengwa ipasavyo. |
| .**Maadili:**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana katika vikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima – mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za vikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa azingatie hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora. |

| 4.0 USAFIRI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa ufasaha**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika matini mbalimbali,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti /ch/ (*k.m chakula, changa, chuma, uchumi, chaki, chifu)* na /dh/ (*k.m dhahabu, fedha*) katika kadi maneno, mti maneno au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno au hadithi yenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo, matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno au hadithi yenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo, sauti inayosikika akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno au hadithi yenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo, kasi ifaayo (maneno 36 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, | Je, ni mambo gani unazingatia kusoma kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ishara zifaazo,<br>f) kufurahia kusoma kifungu ipasvyo ili kufanikisha mawasiliano. | kifaa cha kidijtali, nk akishirikiana na wenzake na kuzingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, nk akishirikiana na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo.<br>● | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia matamshi ya sauti lengwa.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoendelea kusoma vifungu mbalimbali maishani.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi wakati wa shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika kikundi.
- Heshima-mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposoma kifungu chepesi kwa kutumia ishara zifaazo.

**Masuala Mtambuko**

Mshikamano wa kijamii - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali kusoma kifungu cha hadithi kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijaitali.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous language Activities – Masomo haya pia yanashughulikia mada ya kusoma.

| 4.0 USAFIRI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Nafasi katika maandishi.**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nafasi kati ya maneno katika sentensi,<br>b) kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno katika sentensi kwa maandishi,<br>c) kufurahia kuandika akizingatia nafasi kati ya maneno katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua nafasi kati ya maneno katika sentensi akishirikiana na wenzake,<br>• kuwaonyeshe wenzake nafasi kati ya maneno<br>• katika sentensi akishirikiana na wenzake, kuandika sentensi kuhusu suala lengwa akizingatia nafasi kati ya maneno,<br>• kuwaonyesha wenzake sentensi alizoziandika ili wazitolee maoni,<br>• kutumia kifaa cha kidijitali<br>• kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno. | Je, kwa nini tunatumia nafasi kati ya maneno katika sentensi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuonyesha nafasi kati ya maneno katika sentensi.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno kwa kutumia kifaa cha kidijitali.<br>● Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapofanya mazoezi ya ziada ya kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno. |
| **Maadili**<br>● Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Usalama wa watoto barabarani – mwanafunzi anapotunga sentensi sahili zinazohusu mada lengwa ya usafiri hasa usalama barabarani.<br>● Masuala ya fedha – mwanafunzi anapoandika vifungu kuusu matumizi ya fedha katika usafiri. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia stadi ya kuandika |

| 4.0 USAFIRI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Umoja na wingi wa vifungu vya maneno** *(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi,<br>b) kusoma vifungu vya maneno katika umoja na wingi,<br>c) kuandika umoja na wingi wa vifungu vya maneno,<br>d) kuchangamkia kutumia vifungu vya maneno katika umoja na wingi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi (*k.m basi hili - mabasi haya; safari hii - safari hizi; ndege hii - ndege hizi; baiskeli yangu - baiskeli zetu),*<br>● kusoma vifungu vifungu vya maneno katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake, kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali akizingatia suala lengwa,<br>● kuandika umoja na wingi wa vifungu vya maneno akishirikiana na wenzake,<br>● kujaza nafasi zilizo wazi ili kukamilisha vifungu vya maneno katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>● kushiriki katika mchezo wa kupanga kadi za vifungu vya maneno akiambatanisha umoja na | Je, unapozungumzia umoja na wingi wa maneno au sentensi unamaanisha nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wingi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kuandika vifungu vya maneno akiwa na wenzake.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoeleza kuhusu vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Uwajibikaji - mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika shughuli za kikundi.

.**Masuala mtambuko**

- Usalama mtandaoni – mwanafunzi anaposoma kifungu na kutambua maneno ya umoja na wingi kuhusu swala lengwa kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.
- Usalama wa atoto barabarani – wanapotunga sentensi kuhusu suala lengwa la uasifiri.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya yana mada zinazohusu umoja na wingi.

| 5.0 MNYAMA NIMPENDAYE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Hadithi** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha kuhusu suala lengwa,<br>b) kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika hadithi aliyoisikiliza,<br>c) kujibu maswali kuhusu hadithi aliyoisikiliza,<br>d) kueleza ujumbe wa hadithi aliyoisikiliza,<br>e) kufurahia ufahamu wa kusikiliza. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua picha kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kujadili picha kutoka kwenye kitabu, chati, vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi,<br>● kusikiliza ufahamu kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vyombo vya kidijitali,<br>● kutambua msamiati uliotumika katika ufahamu aliousikiliza akishirikiana na wenzake,<br>● kujibu maswali yanayohusiana na ufahamu aliousikiliza,<br>● kueleza maudhui ya ufahamu aliousikiliza akishirikiana na | Kusikiliza hadithi kwa makini kuna umuhimu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake,<br>● kumsimulie mzazi au mlezi wake hadithi aliyoisikiliza kuhusu suala lengwa naye mzazi kumtolea maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua picha na kujadili ujumbe katika kifungu cha ufahamu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kujifunzia.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotabiri yatakayotokea katika hadithi.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu darasani.
- Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya utunzaji wa wanyama – mwanafunzi anapomsimulia mzazi au mlezi hadithi aliyoisikiliza kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya utunzaji wa wanyama – mwanafunzi anaposikiliza na kusikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanafundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza.

| 5.0 MNYAMA NIMPENDAYE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa ufahamu**<br><br>**(*Vipindi 3*)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu<br>kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza au kutazama nyimbo kuhusu suala lengwa kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutaja masuala ya suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kuimba nyimbo kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 39- 42 na kutambua msamiati wa suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati | Je, ni mambo gani yanayokusaidia kupata ujumbe kwenye vifungu vya ufahamu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akishirikiana na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake, | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi kusoma na kujadili ujumbe katika kifungu kuhusu suala lengwa.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika kikundi.
- Umoja - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya utunzaji wanyama – mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi na kutambua msamiati kuhusu usalama wa wanyama.
- Umasikini – mwanafunzi anaposoma vifungu vinavyozungumzia kuhusu suala lengwa la mnyama nimpendaye.

**Uhusiano na masomo mengine**

- English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu.

| 5.0 MNYAMA NIMPENDAYE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Uakifishi: Matumizi ya Kiulizi**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kiulizi katika maandishi,<br>b) kuandika kiulizi ipasavyo akizingatia umbo lake,<br>c) kutumia kiulizi ipasavyo katika sentensi,<br>d) kufurahia kutumia kiulizi katika maandishi ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua kiulizi katika maandishi kitabuni, kwenye kadi maneno, mti maneno na kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika kiulizi ipasavyo akizingatia umbo lake,<br>● kutumia kiulizi ipasavyo katika sentensi,<br>● kutazama matumizi ya kiulizi kwenye vifaa vya kidijitali,<br>● kuandika kiulizi akitumia kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika sentensi sahili akitumia kiulizi ipasavyo,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi sentensi zenye matumizi yafaayo ya kiulizi alizotunga ili ampe maoni yake . | Je, alama ya kiulizi hutumika vipi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapowaeleza na kuwaonyesha wenzake kiulizi kilipotumiwa katika maneno na sentensi.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kuandika kiulizi katika sentensi akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapotamani kuendelea kuandika kiulizi ipasavyo. |
| **Maadili**<br>● Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wanaposhiriki katika shughuli ya kuandika. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii na kitaifa –mwsanafunzi anapowathamini wenzake kutoka jamii mbalimbali wanaposhirikiana kutambua na kutumia kiulizi ipasavyo.<br>● Usalama wa wanyama – mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu usalama wa mnyama nimpendaye. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya yanafunza matumizi ya kiulizi katika sentensi. |

| 5.0 MNYAMA NIMPENDAYE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Matumizi ya -ako na -enu (*Vipindi* 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi yafaayo ya **-ako** na **-enu** katika kifungu,<br>b) kutumia **-ako** na **-enu** ipasavyo katika sentensi,<br>c) kuthamini matumizi ya **-ako** na **-enu** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusilikiliza kifungu au wimbo unaohusu matumizi ya –**ako** na –**enu** katika kifaa cha kidijitali,<br>• kutambua matumizi ya **-ako** na **-enu** katika kadi za maneno, mti maneno, kapu maneno na vifaa halisi kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>• kumtungia mwenzake sentensi zenye matumizi ya **-ako** na **–enu,**<br>• kusikiliza sentensi zinazotungwa na wenzake zenye matumizi ya **-ako** na **-enu** na kuzitolea maoni,<br>• mwanafunzi awasilishie sentensi zenye kutumia maneno **-ako** na **–enu,**<br>• kuandika sentensi zenye **-ako** na **–enu,**<br>• kujaza nafasi kwa kutumia **-ako** na -**enu** kwa kusaidiwa na mwalimu. | Je,-**ako** na **-enu** hutumiwa wakati gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia –**ako** na **-enu.**<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kutumia **-ako** na **-enu** akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia **-ako** na **-enu** kwa lugha fasaha. |
| **Maadili**<br>● Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapojitolea kumtungia mwenzake sentensi akitumia –**ako** na **-enu.** |
| **Masuala mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo tofauti tofauti kutunga sentensi zenye matumizi yafaayo ya **-ako** na **–enu** akizingatia mada lengwa.<br>● Elimu ya utunzaji wa wanyama – mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu mnyama nimpendaye. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>● English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya hushughulikia mada vivumishi vya vimilikishi |

| 6.0 UKOO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora:** *(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa ipasavyo katika maneno na sentensi,<br>b) kutamka maneno na sentensi zenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/ny/* na */ng/*) katika matini mbalimbali kama vile kadi za maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali akizingatia suala lengwa,<br>● kutamka maneno aliyosikiliza pamoja na mwalimu, kisha kuyatamka akishirikiana na mwenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kuambatanisha silabi ili kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa kuhusu suala lengwa,<br>● kujirekodi akisoma sentensi zilizo na maneno yenye sauti lengwa , akishirikiana | Je, unajua kutamka maneno yapi yenye sauti */ny/* na */ng/*? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na wenzake ajisikilize ili kutathmini matamshi bora,<br>● kushiriki katika tamasha za mashairi na nyimbo au hafla shuleni ili aimarishe matamshi yake kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>● kutumia maneno ya silabi za sauti lengwa kuwasiliana na mzazi au mlezi wake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapojirekodi akisoma sentensi na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotamka sauti lengwa ipasavyo na anapojirekodi.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima – mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za vikundi.

**Masuala mtambuko**

- Mshikamano wa kijamii kitaifa– mwanafunzi anaposhiriki katika tamasha za muziki zenye asili ya jamii mbalimbali anakuza matamshi bora na talanta yake.
- Haki za kijamii – mwanafunzi anaposoma maneno yanayolenga suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora.

| 6.0 UKOO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (*/ny/* na */ng/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 39 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, | Je, unajua maneno yapi yaliyo na silabi za sauti */ny/*,na */ng/*? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | kifaa cha kidijtali, n.k akishirikia na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo kuhusu suala lengwa,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu kwa ufasaha.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake kwenye kikundi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma darasani.

**Masuala mtambuko**

- Haki na majukumu ya kibinadamu– mwanafunzi anapotangamana na wenzake kusoma kifungu chepesi cha hadithi kuhusu suala lengwa akizingtia matamshi bora,kasi ifaayo,sauti inayosikika na ishara zifaazo.
- Utunzi na usalama wa watoto – mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa la ukoo.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous language Activities – masomo haya pia yanashughulikia sauti za lugha.

| 6.0 UKOO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Tahajia Imla** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye maandishi kwa kuzingatia sauti lengwa,<br>b) kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu kwa kuzingatia silabi za sauti lengwa,<br>c) kuandika sentensi sahili kwa kuzingatia silabi za sauti lengwa,<br>d) kufurahia kuandika ipasavyo maneno na sentensi kutokana na imla. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye maandishi akizingatia sauti lengwa (/*ny*/ na /*ng*/),<br>● kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu kitabuni au katika kifaa cha kidijitali akizingatia sauti lengwa,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika maneno mepesi ya silabi tatu akizingatia sauti lengwa na suala lengwa,<br>● kushiriki mchezo wa kuandika maneno na sentensi za imla na wenzake,<br>● kuwasilishia wenzake maneno ya imla ili kuyaandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika maneno atakayosomewa na wenzake daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali, | Je, kwa nini tunahitaji kusikiliza kwa makini tunaposomewa maneno ya kuandika? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kushirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi sahili kutokana na maneno waliyoandika akizingatia suala lengwa,<br>• kuandika daftarini sentensi sahili walizotunga na kumpa mwenzake ili azitolee maoni, kisha mwalimu azisahihishe, | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano– mwanafunzi anapofaulu kuwwasilishia wenzake maneno mepesi ya imla na kuyaandika.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kuandika imla akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoteua maneno ya kuwawasilishia wenzake na anaposhiriki mchezo wa kusomea maneno na sentensi za imla.
- Kujiamini- anapotunga sentensi sahili na kuziandika katika daftari ili zisahihishwe na wenzake, pamoja na mwalimu.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya vikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Mahusiano ya kijamii – mwanafunzi anapotangamana na wenzake darasani katika kuandika maneno na sentensi za imla kuhusu ukoo.
- Haki za watoto – mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu ukoo na masuala kuhusu watoto.

**Uhusiano na masomo mengine**

- English Language Activities na Indigenous Language Activities – Masomo haya yanafunza imla

| 6.0 UKOO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Matumizi ya: (-refu, - kubwa, - tamu***)* (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **-refu, -kubwa, - tamu,**<br>**b)** kutumia**-refu, - kubwa, -tamu** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>**c)** kufurahia kutumia- **refu, - kubwa, -tamu** – katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **-refu, - kubwa, - tamu** kwa kurejelea vitu katika mazingira yake kutoka kwa kitabu, au vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusikiliza matumizi ya**-refu**, **- kubwa, -tamu** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa, wenzake na kwa kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma sentensi zinazotumia maneno-**refu, -kubwa, - tamu** zinazolenga suala lengwa,<br>● kutumia **-refu, -kubwa, -tamu** akiwa na wenzake katika kikundi kurejelea vitu katika mazingira yake kuhusu suala lengwa,<br>● kukamilisha sentensi zenye matumizi ya-**refu, -kubwa, - tamu,**<br>● kujaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia -**refu**, **-kubwa, - tamu** katika sentensi | Je, ni maneno kama gani unayoweza kutumia kuelezea sifa za kitu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuhusu suala lengwa,<br>● kuwasiliana na mlezi au mzazi kwa kutumia-**refu -, - kubwa, -tamu** kuelezea vifaa kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapotumia -**refu, -kubwa, -tamu** akiwa na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza matumizi ya-**refu, - kubwa, -tamu**.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapotumia -**refu, -kubwa, -tamu** akiwa na mzazi au mlezi nyumbani.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia -**refu, -kubwa, na-tamu**.

**Maadili**

- Uwajibikaji– mwanafunzi anapotangamana na wenzake kwa heshima katika shughuli za kikundi.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya vikundi.

**Masuala mtambuko**

- Utangamano wa kijamii – mwanafunzi anapotunga sentensi akishirikiana na wenzake akizingatia mazingira ya nyumbani.
- Haki na majukumu ya kibinadamu – mwanafunzi anapotunga sentensi zinazolenga suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities and Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanafundisha kuhusu maneno ya kuelezea sifa za kitu.

| 7.0 SEBULENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Maagizo** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maagizo mepesi ya hatua mbili yanapotolewa katika miktadha mbalimbali,<br>b) kutoa na kufuata maagizo mepesi ya hatua mbili yanayotumiwa katika miktadha mbalimbali,<br>c) kuchangamkia maagizo katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua maagizo ya hatua mbili *(k.v. nenda ukamwite mwenzako),*<br>• kutazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo mepesi ya hatua mbili kwa kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa,<br>• kushiriki katika kutoa na kufuata maagizo mepesi ya hatua mbili<br>• *(k.v. nenda ukamwite mwenzako),*<br>• kufafanua umuhimu wa maagizo,<br>• kuimba nyimbo na kukariri mashairi yanayohusu maagizo kuhusu suala lengwa. | Kufuata maagizo kuna umuhimu gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala na wenzake wakati wa ujifunzaji katika kikundi.<br>● Uwazaji kwa kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotoa anapoigiza maagizo kulingana na yanavyotolewa.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>● Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki kuimba nyimbo na pia kukariri mashairi kuhusu maagizo. |
| **Maadili**<br>● Amani – mwanafunzi anapofanya kazi katika kikundi na wenzake kwa utulivu.<br>● Haki za kijamii – mwanafunzi anapomtolea mwenzake maagizo yafaayo.<br>● Umoja – mwanafunzi anapofanya kazi na wenzake katika kikundi kwa upole na kuelewana. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo ya hatua mbili kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa.<br>● Utunzi na usalama wa watoto – mwanafunzi anaposikiliza vifungu kuhusu sebuleni na vifaa vya sebuleni. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia dhana ya kusoma kwa ufahamu. |

| 7.0 SEBULENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **7.2 Kusoma** | **7.2.1 Kusoma Kwa ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza au kutazama nyimbo kuhusu Suala lengwa kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutaja anayoyajua kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kuimba nyimbo kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 43 - 46 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v kochi, zulia, meza, kiti, runinga )* akishirikiana na wenzake, kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi | Je, tunawezaje kupata ujumbe katika ufahamu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi vitu vinavyopatikana sebuleni mwao kwa kutumia msamiati aliojifunza.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanapotangamana katika shughuli za kikundi.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa upendo katika shughuli mbalimbali za kikundi.
- Uwajibikaji - mwanafunzi anapoeleza wenzake kuhusu vitu vya sebuleni.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya afya ya kujikinga – mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi na kutambua msamiati wa wa swala lengwa kama zulia,kochi,viti na jinsi ya kuviweka safi ili kuweza kujikinga na maradhi.
- Haki za watoto – mwanafunzi anaposoma ufahamu kuhusu sebuleni na vifaa vya sebuleni.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia hushughulikia kusoma kwa ufahamu.

| 7.0 SEBULENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Liliyopendekezwa** |
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Uhariri** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuhariri katika maandishi,<br>b) kuhariri maandishi yake baada ya kuyaandika,<br>c) kufurahia kuhariri maandishi baada ya kuyaandika ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuhariri katika maandishi kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kujadiliana na wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia katika uhariri,<br>● kuipitia kazi yake baada ya kuiandika ili kuhariri tahajia, nafasi baina ya sauti na maneno pamoja na viakifishi kuhusu suala lengwa,<br>● kushirikiana na wenzake kuhariri kazi aliyoandika,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichohariri ili ampe maoni yake. | Je, kwa nini ni vizuri kusoma kazi uliyoandika na kuirekebisha? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapofaulu kuwaonyesha wenzake nafasi baina ya maneno katika kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapofaulu kuhariri kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi akizingatia nafasi ipasavyo. |
| **Maadili**<br>● Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli ya kuhariri kifungu cha maneno mawili na sentensi fupi.<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapoandika kifungu kifupi kuhusu shughuli zinazofanywa na familia yao wanapojumuika sebuleni.<br>● Haki za watoto – mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu sebuleni na vifaa vya sebuleni. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>● English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia uhariri wa maandishi. |

| 7.0 SEBULENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Liliyopendekezwa** |
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi katika sentensi<br>b) kutumia ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi katika sentensi kwa usahihi<br>c) kuchangamkia matumizi ya ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi, katika | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi, katika kadi maneno, mti maneno kuhusu suala lengwa,<br>• kusikiliza kifungu au wimbo<br>• kuhusu ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi kwenye kifaa cha kidijitali,<br>• kushirikiana na wenzake katika kikundi kukanusha sentensi katika nafsi ya pili, umoja na wingi kuhusu suala lengwa, kwa mfano: *wewe - ulisoma – wewe hukusoma,*<br>• kutunga sentensi zinazoashiria ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi kuusu suala lengwa kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>• kufanya zoezi la kujaza nafasi kwa kutumia nafsi ya pili, umoja na wingi, kwenye kifaa cha kidijitali, | Ukanushaji wa sentensi katika umonja na wingi unahusu nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mawasiliano ya kila siku. | ● kumsomea mzazi au mlezi sentensi alizokanusha katika nafsi ya pili, umoja na wingi ili ampe maoni | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki kumtungia mwenzake sentensi katika kikundi kwa kutumia nafsi ya pili umoja na wingi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapoigiza vitendo vinavyoashiria nafsi ya pili umoja na wingi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anaposikiliza kifungu au wimbo kuhusu ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi kwenye kifaa cha kidijitali.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi zinazoashiria ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake wanapotungiana sentensi kwenye kikundi kwa kutumia ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kukanusha sentensi zilizo katika nafsi ya pili umoja na wingi.
- Umoja – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko**

- Usalama mtandaoni –mwanafunzi anapofanya shughuli ya ukanusho wa nafsi ya pili katika umoja na wingi kuhusu suala lengwa akizingatia hatua za kiusalama katika mtandao.
- Utunzi na usalama watoto – mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia dhana ya nafsi.

| 8.0 USALAMA WANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwaa** |
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Matamshi Bora**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno na sentensi zenye sauti lengwa,<br>b) kutamka maneno na sentensi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (/sh/, /th/) katika matini mbalimbali kama vile kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka maneno aliyosikiliza pamoja na mwalimu na mwishowe kutamka akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kuambatanisha silabi ili kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye sauti lengwa na zinazolenga suala lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kuzitambua, | Unajua kutamka maneno gani yenye sauti /sh/ na /th/? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kusikiliza kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa na kutambua sauti lengwa,<br>● asimulie kifungu cha hadithi kinacholenga sauti lengwa na suala lengwa,<br>● kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno na sentensi zenye sauti lengwa na kujisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi bora. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapojirekodi akisimulia kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotamka sauti lengwa ipasavyo.

**Maadili**

- Umoja – wanafunzi wanaposhirikiana katika vikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za vikundi.

**Masuala mtambuko**

- Utunzi wa usalama wa watoto – mwanafunzi anaposikilia kifungu cha hadithi kinacholenga mada lengwa na kutambua maneno yenye sauti /*sh*/na /*th*/.
- Magonjwa yanayosababishwa na mitindo ya maisha – mwanafunzi anaposikiliza kifungu kinacholenga suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia dhana ya matamshi bora.

| 8.0 USALAMA WANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa ufasaha**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti /*sh*/ na /*th*/ katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwak wa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kw kuzingatia kasi ifaayo (maneno 42 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, | Je, unajua kusoma maneno gani yenye sauti /sh/ na /th/? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kifaa cha kidijtali, n.k. akishirikiana na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoendelea kusoma sentensi na vifungu mbalimbali vyenye sauti lengwa.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake kwenye kikundi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.

**Masuala mtambuko**

- Utunzi na usalama wa watoto - mwanafunzi anaposoma kifungu kinachohusu suala lengwa, anakuza ujuzi wake kuhusu masuala ya usalama.
- Afya ya mtu binafsi – mwanafunzi anaposoma vifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma vifungu.

| 8.0 USALAMA WANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Tahajia**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tahajia sahihi za maneno katika sentensi,<br>b) kuandika sentensi akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>c) kufurahia kutumia tahajia sahihi katika maandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua tahajia sahihi za maneno katika sentensi kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili kuhusu tahajia sahihi ya maneno kwenye kifungu kitabuni au kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika sentensi kuhusu suala lengwa akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>● kurekebisha sentensi akizingatia tahajia sahihi,<br>● kujaza nafasi kwenye kifungu akizingatia tahajia sahihi kinachozungumzia suala lengwa,<br>● kumsomea mzazi au mlezi sentensi alizotunga akizingatia tahajia sahihi ili ampe maoni. | Je, kwa nini ni vizuri kuandika maneno kwa kuzingatia tahajia ifaayo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuchangia kikamilifu katika kutambua na kuandika akizingatia tahajia sahihi.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kuandika sentensi zinazozingatia tahajia akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapofaulu kutumia tahajia sahihi katika sentensi. |
| **Maadili**<br>● Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Usalama wa watoto barabarani – mwanafunzi anapotambua tahajia sahihi za maneno katika sentensi kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali akizingatia mada lengwa.<br>● Haki za watoto – mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya yanafunza pia tahajia. |

| 8.0 USALAMA WANGU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Matumizi ya huu na hii**<br><br>*(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua **huu** na **hii** katika vifungu,<br>a) kutumia **huu** na **hii** kutajia vitu katika mazingira yake,<br>b) kuchangamkia matumizi ya **huu** na **hii** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno **huu** na **hii** kwa kutumia nyenzo kama vile kadi maneno, mti maneno, chati au kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma vifungu vinavyojumuisha **huu** na **hii,**<br>● kuonyesha vitu mbalimbali kuhusu suala lengwa kama vile miti na kuvitungia sentensi katika kikundi k.m *Mti huu – miti hii,*<br>● kukamilisha vifungu vyenye nafasi kwa kutumia **huu** na **hii** akishirikiana na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia **huu** na **hii** na zinazolenga suala lengwa**,** kuandika vifungu akitumia **huu** na **hii** kutokana na picha. | Ni vitu gani unavyoweza kurejelea kwa kutumia maneno **huu** na **hii**? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua maneno **huu** na **hii** na kutunga sentensi akiyatumia.<br>● Hamu ya ujifunzaji – anapomshirikisha mzazi au mlezi wake kurejelea vitu vinavyopatikana nyumbani kwa kutumia maneno **huu** na **hii** ipasavyo.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kiteknolojia kujifunzia. |
| **Maadili**<br>Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Magonjwa ya kuambukizwa na yasiyoambukizwa – mwanafunzi anapoandika kifungu chepesi kuhusu usalama wangu akitumia **huu** na **hii** kutokana na picha ipasavyo.<br>● Haki za watoto – mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya yana mada kuhusu vionyeshi |

| 9.0 HOSPITALINI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo ya papo kwa hapo** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kuonyesha ufahamu wa suala inalozungumziwa,<br>b) kuzingatia matamshi bora anapozungumza,<br>c) kujieleza kwa ufasaha wakati wa kuzungumza,<br>kutumia viziada lugha ipasavyo wakati wa kuzungumza,<br>d) kufurahia kutoa mazungumzo ya papo kwa papo ili kujenga ufasaha wa kuzungumza. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kuonyesha ufahamu wa suala lengwa kwa kulieleza ipasavyo<br>● kusikiliza mgeni mwalikwa au mwalimu, wakizungumza,<br>● kushirikiana na wenzake kusikiliza mazungumzo kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa,<br>● kuzungumza kwa kutamka ipasavyo sauti na maneno,<br>● kujieleza kwa ufasaha anapozungumza kwa kutumia lugha inayoeleweka kuhusu suala lengwa,<br>kutumia sauti ipasavyo kwa kuzingatia sauti inayosikika, kasi ya kuzungumza, toni pamoja na udhibiti wa upumuaji na viungo | Tunazingatia mambo gani tunapozungumza papo kwa hapo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vya kutamka,<br>● kuzungumza akitumia ipasavyo viziada lugha kama vile muktadha wa mazungumzo, ishara (za uso, mikono) mtuo, mkao wa mwili, utazamaji hadhira kuhusu suala lengwa,<br>● kushirikiana na wenzake kuwasilisha mazungumzo ya papo kwa papo wakiwa na wenzake, au wakati wa mazungumzo ya hadhara katika tamasha za muziki. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuwasilisha hoja zake.<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapofanikiwa kuwasilisha mazungumzo yake ifaavyo mbele ya wenzake.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali kujifunzia.<br>● Uraia – mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Maadili**<br>● Upendo – mwanafunzi anapowapatia wenzake nafasi kushiriki katika majadiliano.<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali na kukitunza ipasavyo. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Elimu ya afya ya kujikinga – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusikiliza mazungumzo yanayohusu afya na jinsi ya kuepuka maradhi mbalimbali. |

| |
| --- |
| • Haki za watoto – mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya yanafundisha dhana ya kusikiliza na kuzungumza. |

| 9.0 HOSPITALINI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama na wenzake picha au michoro ya hospitali kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali,<br>● kuimba nyimbo kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 47 - 50 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v hospitali, tibu, daktari, mgonjwa, sindano, dawa, ugonjwa, afya, wodi, machela, bendeji)* akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu kuhusu suala lengwa | Je, ukitaka kupata ujumbe kwenye kifungu unazingatia nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akishirikiana na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe na mafunzo katika kifungu cha ufahamu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomhadithia mzazi au mlezi kifungu alichokisoma shuleni kuhusu suala lengwa.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanaposhiriki katika shughuli za kikundi.
- Upendo – mwanafunzi anapowajali wenzake katika kikundi na kuwapa nafasi ya kushiriki.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya afya ya kujikinga – mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi cha ufahamu kuhusu suala lengwa.
- Afya mtu binafsi- mwanafunzi anaposoma kifungu kuhu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities - masomo haya pia yanazingatia kusoma kwa ufahamu.

| 9.0 HOSPITALINI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Kuandika Kifungu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua suala la kuandikia kifungu,<br>b) kuandika kifungu kifupi kutokana na mazingira yake,<br>c) kufurahia kuandika kifungu ili kujieleza. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua suala la kuandikia kwa kulijadiliana na wenzake darasani,<br>● kutazama picha kuhusu suala lengwa ili kupata habari za kuandikia,<br>● kuwaelekeza wenzake kuhusu atakachoandikia wakiwa au na wenzake,<br>● kusikiliza wenzake wakieleza kuhusu jambo au suala watakaloandikia kuhusu suala lengwa,<br>● kuandika kifungu kifupi cha sentensi moja au zaidi chenye maelezo yanayoeleweka kuhusu suala lengwa,<br>● kuwawasilishia wenzake kifungu alichoandika ili wakitolee maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu | Je, unaongozwa na mambo gani unapotaka kuandika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | alichokiandika na kumweleza suala aliloandikia ili ampe maoni | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu suala la kuandikia.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kutumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kujadili suala analoliandikia.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya afya ya kujikinga – mwanafunzi anapoandika kifungu kifupi kutokana na mazingira yanayohusu suala lengwa.
- Afya ya mtu binafsi – mwanafunzi anapoandika kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

- English Language Activities na Indigenous Language Activities – Masomo haya pia yanafunza stadi ya kuandika.

| 9.0 HOSPITALINI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Matumizi ya vizuri na vibaya, polepole** na **haraka** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi yafaayo ya **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** katika kifungu,<br>b) kutumia **vizuri** na **vibaya, polepole** na **haraka** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **vizuri** na **vibaya** katika kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** katika nyenzo kama vile kadi za majina, kapu maneno, mti maneno au chati,<br>● kuigiza vitendo mbalimbali kwa kutumia **vizuri** na **vibaya, polepole** na **haraka** k.m *Maria anasoma vizuri; daktari alimtibu vizuri; Mbuzi aliruka vibaya; Mwalimu anatembea polepole; mgonjwa alipona haraka,*<br>● kuandika sentensi zinazojumuisha **vizuri** na **vibaya, polepole** na **haraka,**<br>● kujaza nafasi kwa kutumia **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** akizingatia suala lengwa kwa kusaidiwa na mwalimu. | Unatumia maneno yapi kuelezea jinsi watu wanavyofanya vitendo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka**.<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka**.<br>● Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapowasiliana na mzazi au mlezi kwa kutumia vielezi **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** kurejelea vitendo anavyofanya nyumbani. |
| **Maadili**<br>● Heshima – mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **vizuri** na **vibaya**, **polepol**e na **haraka**.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapojitolea kuwasiliana na mzazi au mlezi kwa kutumia vielezi **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** kurejelea vitendo anavyofanya nyumbani.<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza matumizi ya vitendo anavyofanya nyumbani kwa kutumia vielezi **vizuri** na **vibaya**,**polepole** na **haraka**. |
| **Masuala mtambuko**<br>● Elimu ya afya ya kujikinga – mwanafunzi anapotumia **vizuri** na **vibaya** , **polepole** na **haraka** kutunga sentensi akizingatia suala lengwa.<br>● Afya ya mtu binafsi – mwanafunzi anapotunga sentensi kwa kuzingatia suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia hushughulikia suala la vielezi |

| 10.0 HALI YA ANGA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti mbalimbali za Kiswahili kwa ufasaha,<br>c) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti za alfabeti ya Kiswahili (a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i j, k, l, m, n, ng, ng', ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z) katika matini mbalimbali au kifaa cha kidijitali,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti mbalimbali za Kiswahili yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali yanayolenga suala lengwa,<br>● kutamka pamoja na mwalimu maneno aliyosikiliza, kisha ayaseme akishirikiana na wenzake akilenga suala lengwa,<br>● kuunganisha silabi ili kusoma maneno yanayotokana na sauti mbalimbali,<br>● kujirekodi akisoma maneno yenye sauti mbalimbali za Kiswahili na kujisikiliza | Unazingatia nini kutamka sauti za Kiswahili kikamilifu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na wenzake ili kutathmini matamshi bora. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti mbalimbali.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti mbalimbali.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili.
- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anapotambua sauti za alfabeti ya Kiswahili katika matini mbalimbali kuhusu suala lengwa.
- Haki na majukumu ya kibinadamu – mwanafunzi anapotumia maneno yanayolenga suala mtambuko.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia dhana ya matamshi bora.

| 10.0 HALI YA ANGA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa ufasaha** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti mbalimbali za Kiswahili katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa sauti inayosikika akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 45 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake,<br>● kuwawasilishia hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, nk | Kusoma kifungu kwa kwa ufasaha unazingatia mambo gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akishirikiana na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi walichosoma shuleni kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi walichosoma shuleni kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikiia, kasi na ishara zifaazo.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutekeleza shughuli mbalimbali za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.
- Haki na majukumu ya kibinadamu – mwanafunzi anaposoma vifungu vinavyolenga suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia mada ya kusoma.

| 10.0 HALI YA ANGA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Maneno Na Sentensi**<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye matini mbalimbali,<br>b) kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu yanayohusu suala lengwa,<br>c) kuandika sentensi fupi zinazohusu suala lengwa,<br>d) kufurahia kuandika ipasavyo maneno na sentensi kutokana na imla. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye matini mbalimbali,<br>● kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu kitabuni au katika kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika maneno mepesi ya silabi tatu,<br>● kushiriki mchezo wa kuandika maneno na sentensi za imla akiwa na wenzake yanayolenga suala lengwa,<br>● kuwawasilishia wenzake maneno ya imla ili kuyaandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika maneno atakayosomewa na wenzake ili kuandika daftarini au kwenye | Sentensi sahili ni sentensi za aina gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika daftarini sentensi sahili walizotunga zinazolenga suala lengwa,<br>● kusahihisha kazi yake na wenzake, | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutambua maneno ya silabi tatu katika sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapoandika akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoandika sentensi za imla akishirikiana na mzazi au mlezi kwenye kifaa cha kidijitali na kuwatumia wenzake mtandaoni.
- Ubunifu – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuunda sentensi nyepesi.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anapoandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu yanayohusu suala lengwa.
- Magonjwa ya kuambukizwa na yasiyoyakuambukizwa – mwanafunzi anapoandika sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya yanafunza kuandika.

| 10.0 HALI YA ANGA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya vitendo** (vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitendo katika sentensi mbalimbali,<br>b) kutumia majina ya vinyume vya vitendo katika sentensi,<br>c) Kuchangamkia kutumia majina ya vinyume vya vitendo katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vinyume vya vitendo katika sentensi *(k.v,Maria amesimama- Maria ameketi,Funga mlango-Fungua mlango, Mtoto amelala- Mtoto ameamka)* katika kadi maneno. kapu maneno, kifungu, chati, kitabu au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake akizingatia suala lengwa,<br>● kusikiliza sentensi zenye vinyume vya vitendo zikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma vinyume vya vitendo katika sentensi vinavyohusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa katika sentensi akiwa na wenzake,<br>● akamilishe sentensi akitumia vinyume vya vitendo akishirikiana na wenzake, | Je, vinyume vya vitendo huwa vinahusu nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | - kutunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni,<br>- kumsomea mzazi au mlezi sentensi alizotunga kwa kutumia vinyume vya vitendo ili ampe maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano -mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuandika vinyume vya vitendo katika sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya teknolojia kusikiliza matumizi ya vinyume vya vitendo.
- Ubunifu – anapoigiza matumizi ya vinyume vya vitendo mbalimbali.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko**

- Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumika katika sentensi
- Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo vinavyohusiana na hali ya anga.

**Uhusiano na masomo mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya yana mada kuhusu vinyume.

**MWONGOZO WA KUTATHMINIA STADI ZA LUGHA GREDI YA 2**

| STADI YA KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kiwango** <br> **Kigezo** | **Kuzidi Matarajio Kiwango 4** | **Kufikia Matarajio Kiwango 3** | **Kukaribia Matarajio Kiwango 2** | **Mbali Na Matarajio Kiwango 1** |
| **Kuweza kuwasiliana kwa njia ifaayo** (*matamshi, kiimbo na kusikika*) | Mwanafunzi anajieleza kwa ufasaha na urahisi, bila makosa ya kimatamshi ya sauti lengwa na anapozungumza anasikika ipasavyo na asemayo yanaeleweka vyema. Maelezo yake yana mantiki na yanafuatilika kwa urahisi. Anazungumza kama mzawa wa lugha hii. | Mwanafunzi anajieleza kwa ufasaha. Ana matamshi yafaayo yanayozingatia sauti lengwa . Aidha ana kiimbo mwafaka. Ana makosa machache ya kimatamshi na kiimbo lakini anasikika vyema na asemayo yanaeleweka. | Mwanafunzi anajieleza kwa kusitasita. Anafanya makosa ya kimatamshi yanayotokana na sauti lengwa na kiimbo chake kina udhaifu. Mara kwa mara na hasisikiki vyema. Maana inaweza kukisiwa kutokana na asemayo. | Ana stadi hafifu za kimatamshi na kiimbo. Anafanya makosa mengi ya kimatamshi. Anakosa mantiki /mfuatano ufaao katika kujieleza. Hasisikiki vyema na asemayo hayaeleweki. |
| **Kufahamu suala lengwa** (*majibu sahihi, matumizi ya msamiati mwafaka*) | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa kulingana na maagizo katika mazingira yake. Anatoa majibu sahihi kwa maswali yote | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa kulingana na maagizo katika mazingira yake. Anatoa majibu sahihi kwa idadi kubwa ya | Anatoa maelezo kwa baadhi ya maswali katika muktadha kulingana na maagizo katika mazingira yake. Anatoa majibu kwa | Ana changamoto kufuata maagizo na kuelewa maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. Anautumia msamiati |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | aliyoulizwa kwenye muktadha. Anautumia msamiati mpana wa mada lengwa kwa usahihi. | maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. Anatumia msamiati lengwa ipasavyo k.m hiki na hivi. | baadhi ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. Anatumia baadhi ya msamiati wa suala lengwa. | finyu wa mada lengwa. |
| **Kutumia msamiati wa suala lengwa** *(msamiati wa heshima, adabu, maamkuzi, maagano, n.k)* | Anatumia msamiati mbalimbali kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. Kwa mfano hiki na hivi. | Anatumia msamiati mwafaka kulingana na muktadha/suala lengwa. Kwa mfano hiki na hivi. | Anatumia msamiati mchache kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. Kwa mfano hiki na hivi. | Anatumia msamiati wa mada lengwa kwa kutatizika ana changamoto kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. |
| **Kutumia ishara za mwili ipasavyo (***jinsi anavyoketi/kusimama, ishara uso, kumtazama mwalimu,ukakamavu)* | Anaketi/ kusimama na kutumia ishara za uso na mwili ipasavyo. Anamtazama mwalimu kila wakati kwa nia ya kuwasilisha ujumbe na anazungumza kwa ukakamavu. | Anaketi/ kusimama na kutumia ishara za uso na mwili ipasavyo. Anamtazama mwalimu wakati mwingi kwa nia ya kuwasilisha ujumbe na anazungumza kwa ukakamavu. | Anaketi/kusimama na kutumia baadhi ya ishara za uso na mwili. Anamtazama mwalimu mara kwa mara na anazungumza kwa kusitasita. Baadhi ya nyakati anazungumza kwa ukakamavu. | Ni nadra sana kutumia ishara za uso na mwili. Hamtazami mwalimu kabisa. Anaangalia chini au kando akizungumza. |

| STADI YA KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kiwango**<br><br>**Kigezo** | **Kuzidi Matarajio**<br><br>**Kiwango 4** | **Kufikia Matarajio Kiwango 3** | **Kukaribia Matarajio Kiwango 2** | **Mbali Na Matarajio Kiwango 1** |
| Kuzingatia jinsi ya kuketi na mbinu zifaazo wakati wa kusoma. *(kuketi wima, kushika kitabu ipasavyo, kuelekeza macho kutoka kushoto hadi kulia n.k)* | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kusoma. Anatumia vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo bila ugumu wowote. Anatumia ishara za mwili kwa njia mwafaka anaposoma kwa wepesi. | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kusoma. Anatumia vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo. Anatumia ishara za mwili kwa njia mwafaka anaposoma. | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kusoma. Anatumia baadhi ya vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo. Anatumia baadhi ya ishara za mwili kwa njia mwafaka anaposoma | Anachangamoto ya kuketi jinsi inavyofaa wakati wa kusoma. Anatumia baadhi ya vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo kwa usaidizi. Anatumia ishara chache za mwili kwa njia mwafaka anaposoma |
| **Kufahamu suala lengwa** *(majibu sahihi, matumizi ya msamiati mwafaka, anwani, picha na michoro*) | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa alilosoma kwenye matini kwa urahisi. Anatoa majibu sahihi kwa maswali yote aliyoulizwa kwenye muktadha. | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa alilosoma kwenye matini. Anatoa majibu sahihi kwa idadi kubwa ya maswali aliyoulizwa | Anatoa maelezo kwa baadhi ya maswali katika muktadha. Anatoa majibu kwa baadhi ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. | Anachangamoto kuelewa na kutoa maelezo kwa maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kulingana na muktadha | | |
| Kusoma kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia kipengele cha ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha na urahisi. | Anasoma kwa kuzingatia kipengele cha ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele k.m ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu. | Anajaribu kusoma sehemu za kifungu bila kuzingatia kipengele cha ujumbe, matukio na wahusika. |
| **Kasi ya usomaji** (*Idadi ya maneno yanayosomwa kwa usahihi kwa muda wa dakika moja*) | Anasoma kwa urahisi na mfululizo wakati wote. Anatumia vituo/ alama za uakifishaji mahali panapofaa wakati wote anaposoma kifungu kuanzia mwanzo hadi mwisho. Anasoma kwa usahihi zaidi ya maneno **(39-42** kwa muda wa dakika moja. | Anasoma kwa urahisi na mfululizo. Anatumia vituo/ alama za uakifishaji mahali panapofaa katika kiasi kikubwa cha muda wa kusoma. Anasoma kwa usahihi idadi ifaayo ya maneno **(39-42)** kwa muda wa dakika moja. | Wakati mwingine anasitasita anaposoma. Hazingatii kikamilifu vipumuo na vikomo mwishoni mwa sentensi. Anasoma kwa usahihi kati ya maneno **(19-21)** kwa muda wa dakika moja. | Anatatizika kusoma na anarudiarudia maneno mengi na inabidi kurudi nyuma kuanza upya. Anachosoma hakiwezi kufuatilika. Anasoma kwa usahihi kati ya maneno **(8-11)** kwa muda wa dakika moja. |

| STADI YA KUANDIKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kiwango**<br><br>**Kigezo** | **Kuzidi Matarajio**<br><br>**Kiwango 4** | **Kufikia Matarajio Kiwango 3** | **Kukaribia Matarajio Kiwango 2** | **Mbali Na Matarajio Kiwango 1** |
| Kuzingatia jinsi ya kuketi na mbinu zifaazo wakati wa kuandika. *(kuketi wima, kushika kalamu, ipasavyo, kuandika kutoka kushoto hadi kulia n.k)* | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kuandika Anatumia vifaa vya kuandika kwa namna ifaayo bila ugumu wowote. | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kuandika. Anatumia vifaa vya kuandika. kwa namna ifaayo. | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kuandika. Anatumia baadhi ya vifaa vya kuandika. kwa namna ifaayo. | Anachangamoto ya kuketi jinsi inavyofaa wakati wa kuandika. Anatumia baadhi ya vifaa vya kuandika kwa namna ifaayo kwa usaidizi. |
| Kuandika sentensi au kifungu kifupi kwa kuzingatia mada lengwa | Anaonyesha ubunifu na uasilia mkubwa katika uandishi wa sentensi kwa kuzingatia mada lengwa. | Anaandika sentensi kwa ubunifu kwa kuzingatia mada lengwa. | Anaandika sentensi kwa ubunifu kwa kuzingatia mada lengwa. | Ana changamoto kuandika sentensi kwa kuzingatia mada lengwa. |
| Kuandika kwa hati nzuri | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi. Anatenganisha herufi zote ipasavyo | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi. Anatenganisha herufi nyingi | Ana mwandiko usio nadhifu lakini unasomeka. Anatenganisha baadhi ya herufi | Ana mwandiko usiosomeka kwa urahisi. Hatenganishi herufi nyingi ipasavyo. Anaacha nafasi nyingi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kwenye mistari. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno kutoka mwanzo hadi mwisho wa insha. | ipasavyo. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno. | ipasavyo. Anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno. | zisizolingana baina ya maneno. |
| Msamiati | Ana uteuzi mzuri wa maneno na matumizi anuwai ya msamiati kulingana na muktadha wa sentensi. | Ana uteuzi mzuri wa msamiati anaoutumia katika kutunga sentensi. | Anatumia msamiati finyu ambao wakati mwingi haulingani na muktadha wa sentensi. | Anatumia msamiati finyu ambao haulingani na muktadha wa sentensi. |
| Kuzingatia muundo na mtindo wa kuandika na kuhariri sentensi au matini (uakifishaji ufaao) | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu | Anachangamoto kuzingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu |

## MWONGOZO WA KUTATHMINIA SARUFI

| Kigezo | Kuzidi Matarajio Kiwango 4 | Kufikia Matarajio Kiwango 3 | Kukaribia Matarajio Kiwango 2 | Mbali Na Matarajio Kiwango 1 |
|---|---|---|---|---|
| **Kutambua aina za maneno katika lugha ya Kiswahili *(wewe, nyinyi , huyo, hawa, ako, enu n.k)*** | Anatambua aina za maneno aliyofunzwa katika matini alizopewa kwa wepesi | Anatambua aina za maneno aliyofunzwa katika matini alizopewa | Anatambua aina za maneno aliyofunzwa katika matini alizopewa. | Anachangamoto kutambua aina za maneno aliyopewa katika matini alizopewa. |
| **Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno aliyofunzwa** | Anatunga sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyofunzwa kwa wepesi | Anatunga sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyopewa kwa ipasavyo. | Anatunga baadhi ya sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyopewa. | Anatunga baadhi ya sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyopewa kwa kuelekezwa |
| **Kutumia lugha kwa usahihi** *(uakifishaji, ukanushaji wa nafsi ya pili, umoja, wingi, udogo, n.k)* | Anazingatia kanuni za lugha ipasavyo katika matini kwa utendeti. | Anazingatia kanuni za lugha ipasavyo katika matini. | Anazingatia baadhi ya kanuni za lugha ipasavyo katika matini. | Anazingatia kanuni baadhi y kanuni za lugha ipasavyo katika matini kwa kuelekezwa. |

## APPENDIX I: SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL)

Katika kiwango hiki, lengo la shughuli ya CSL ni kuambatanisha dhana zilizofunzwa darasani katika masomo mbalimbali na tajriba za maisha halisi. Huwawezesha wanafunzi kuona jinsi mambo waliyojifunza yanavyohusiana na maisha ya kila siku. CSL huwa katika somo la *Environmental Activities*. Mwalimu darasani anatarajiwa kutambua na kuwaelekeza wanafunzi kutekeleza shughuli ya CSL ya darasa zima na jumuishi inayofaa kulingana na umri wa wanafunzi ndani ya shule. Usalama wa wanafunzi unafaa utiliwe maanani wakati wa kuchagua shughuli hii. Zifuatazo ni hatua za shughuli ya CSL jumuishi ambayo inafaa itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula wa shule.

| **Hatua za utekelezaji wa CSL jumuishi** |
|---|
| **1. Maandalizi**<br>• Amua shughuli itakayotekelezwa na wanafunzi.<br>• Tambua umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo mahususi kwa shughuli ya CSL.<br>• Tambua nyenzo hitajika kwa shughuli hiyo (vifaa vinavyopatikana karibu).<br>• Panga shughuli hiyo itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula (weka tarehe na saa ya shughuli).<br>• Wasiliana na wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule, walimu na wadau wengine katika jamii ya shule.<br>• Tambua na ukuze vifaa vya kutathminia. |
| **2. Utekelezaji wa shughuli ya CSL**<br>• Wapatie wanafunzi majukumu.<br>• Hakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki katika shughuli hii.<br>• Watazame wanafunzi wanapotekeleza shughuli ya CSL na uweke rekodi ya matokeo.<br>• Tumia kifaa kifaacho cha tathmini kutathmini mchakato wa shughuli na matokeo (tathmini kazi ya wanafunzi kutoka mwanzo hadi mwisho).<br>• Tathmini umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo. |

3. **Utafakuri wa shughuli ya CSL**
   Kuwa na muda wa tathmini binafsi na wanafunzi kuhusu shughuli waliyotekeleza ya CSL jumuishi kwa kujadili yafuatayo:
   - Ni nini kilifanyika vyema na kwa nini.
   - Ni nini ambacho hakikufanyika vizuri na kwa nini.
   - Ni nini kinachoweza kufanywa kwa njia tofauti wakati ujao.
   - Ni nini wanafunzi walijifunza.

Kutakuwa na shughuli moja ya CSL kwa mwaka. Masuala makuu ya CSL jumuishi yatatokana na kategoria pana za masuala mtambuko na ujuzi unaolengwa katika masomo mbalimbali. Walimu wanatarajiwa kuwa na masuala tofautitofauti yanayolengwa kila mwaka ili kuwapa fursa wanafunzi kutalii masuala mtambuko mbalimbali. Kunafaa kuwa na uhusiano kati ya stadi za masomo na masuala makuu.

Shughuli ya CSL jumuishi itakuwa ya shule nzima ambapo jamii yote ya shule itahusika (wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule na walimu). Wazazi/walezi ni washikadau muhimu katika kupanga na kutekeleza shughuli ya CSL. Ingawa walimu huongoza upangaji na utekelezaji wa shughuli ya CSL, wanafunzi watatarajiwa kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.

Shughuli hii ya CSL hutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili mbalimbali. Mwalimu anatarajiwa kulenga umilisi na maadili tofautitofauti.

**Tathmini ya shughuli ya CSL**
Tathmini ya CSL jumuishi italenga vipengele 3 ambavyo ni: stadi kutokana na masomo mbalimbali yatakayojumuishwa katika shughuli hii, umilisi wa kimsingi uliokuzwa na maadili yaliyokuzwa. Tathmini inafaa kulenga mchakato mzima wa utekelezaji na matokeo ya mwisho ya shughuli. Mwalimu atatathmini wanafunzi katika vikundi akitumia vifaa mbalimbali kama vile ratiba ya ukaguzi, orodha hakiki, kiwango cha ukadiriaji na vifaa vingine faafu vya tathmini.